**Learning by Ear – Hygiene: How to avoid diarrhoea**

**Episode 10** **"Jamii zetu"**

**Author:** **Njoki C. Muhoho**

**Medical Advisor** **Dr Ng'ethe Muhoho**

**Editor** **Maja Braun**

**KISUAHELI** **ERIC PONDA**

<table>
<tr><th>Scene</th><th>Characters</th><th></th></tr>
<tr><td>1</td><td>1. SAM<br>2. CHEMU<br>3. EDITH<br>4. MARIA<br>5. EDDI<br>6. NARRATOR</td><td rowspan="4">SAM – 17, m<br>MARIA – 43, f.<br>EDITH – 40, f.<br>EDDI – 36, m.<br>DR SALLY – 34, f.<br>CHEMU – 15, f.<br>CHIEF – 60, m.<br>CROWD<br>HEADMASTER – 45, m.<br>NARRATOR</td></tr>
<tr><td>2</td><td>1. SAM<br>2. CHEMU</td></tr>
<tr><td>3</td><td>1. SAM<br>2. CHEMU<br>3. EDDI</td></tr>
<tr><td>4</td><td>1. SAM<br>2. CHEMU</td></tr>
</table>

**INTRO**

**MUSIC: THEME MUSIC**

**01. NARRATOR** HUJAMBO NA KARIBU KWA MAKALA HII YA KUMI NA YA MWISHO YA MFULULIZO WA VIPINDI VYA NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO KUHUSU MASUALA YA USAFI NA KINGA DHIDI YA UGONJWA WA KUHARA. KATIKA MCHEZO HUU SAM NA CHEMU WANAJIFUNZA MENGI KUHUSU DALILI, CHANZO, KINGA NA TIBA YA UGONJWA WA KUHARA.NA HIVI LEO KATIKA MAKALA HII YA MWISHO, WAWILI HAO PAMOJA NA FAMILIA ZAO WANAISAMBAZIA JAMII NZIMA HABARI HIZI, KWANI KAMA TUJUAVYO JUHUDI ZA KUDUMISHA USAFI NI WAJIBU WA KILA MMOJA KATIKA JAMII.

ENDELEA KUWA NASI HADI TAMATI ILI NAWE UPATE KUJIFUNZA JINSI UNAVYOWEZA KUISHIRIKISHA JAMII YAKO KATIKA JUHUDI ZA KUZIPUNGUZA ATHARI ZA UGONJWA WA KUHARA..

**SCENE 1: MARIA'S HOME COMPOUND**

**02. *SFX: SOUND OF CUTLERY***

**03. SAM** Shangazi Maria, ahsante sana kwa kiamsha kinywa kizuri.

**04. *SFX: LOUD KNOCK ON THE DOOR***

**05. EDITH** (***from outside)*** Maria, Maria; bado mnakunywa chai na hao watoto? Tutachelewa….

**06. MARIA** Edith, karibu ndani. Unahitaji kunywa chai pia.

**07. *SFX: DOOR OPENS AND SLAMS SHUT***

**08. EDITH** Maria, Eddi na mkewe Sally watawasili sasa hivi.. fanyeni haraka!.

**09. MARIA** Edith keti kidogo unywe chai. Una wasi wasi kuhusu mkutano huu. Hatujachelewa!Bado tuna muda.

**10. SAM** Nafurahi hatimaye Chifu amekubali kutuunga mkono.

**11. EDITH** Kuna umuhimu mkubwa wa kubadilishana mawazo kuhusu ugonjwa huu wa kuhara katika jamii.

**12. CHEMU** Na ni lazima tuwafunze wimbo wetu!. *(raps)*

*Wash your hands.*
*Only washed hands*
*should be used,*
*to eat.*
*Careless people,*
*Don't wash their hands*
*after visiting the toilet.*
*Keep healthy.*
*Wash your hands.*

**13. SAM** Na nyinyi je…? Mama na shangazi Maria. Pia ni lazima mjifunze wimbo huu vile vile!..

**14. MARIA** Mimi? eti ni Rap? Vijana ndio hu-Rap, lakini sisi kina mama ni kuimba tu. Tumepitwa na wakati .... ehhh Ku-Rap.

**15. EDITH** Nina wazo Maria. Kwanini tusiutungie sauti wimbo huu, kisha wakati watoto wanapoanza *Ku-Rap* tunaweza pia kuimba pamoja nao. Lazima tujifunze..!. Nani anayejali iwapo ni sauti nzuri au mbaya, cha msingi ni ujumbe umfikie anayekusudiwa**.**

**16. MARIA** Anza basi…. endelea kunifunza…

**17. SAM AND CHEMU** ***(Chidding)*** Ndio Mama!…Ndio!

**18. EDITH** ***(Making up a tune)***

*Wash your hands.*
*Only washed hands*
*should be used,*
*to eat.*

**19. SAM/CHEMU** **(*CLAP IN RHYTHM)***

**20. EDITH/MARIA** ***(joins in, though off tune, she tries to carry the tune)***

*Careless people,*
*Don't wash their hands*
*after visiting the toilet.*
*Keep healthy.*

**21. SAM/CHEMU (*CHEER AND CLAP HANDS)***

**22. CHEMU** ***(cheering)*** Mama wimbo mzuri sana ..umejaribu…., japo umeikosea sauti, lakini umejitahidi…

**23. *SFX (FROM OUTSIDE) A CAR DRIVES UP AND HOOTS.***

**24. EDITH** Eddi na Sally wamefika, twendeni sasa!.

**25. *SFX: CHAIRS SQUEAK AS THEY LEAVE. DOOR OPENS AND SHUTS, OUTSIDE SOUNDS: BIRDS***

**26. EDDI** ***(cheerfully)*** Habari za asubuhi Mama Sam na wengine nyote. Je kila mmoja yuko tayari kwa siku hii muhimu?

**27. EDITH** Tunaendelea vizuri Eddi. Tunafurahi kwamba wewe na Sally mumefika.Sasa twendeni sije Chifu akatusubiri kwa muda mrefu .Twendeni Eddi

**28. MARIA** Tunachelewa Eddi , twendeni! Lazima ukumbi utakuwa umejaa sasa.

**29. NARRATOR** KULIKONI? NI KWANINI EDDI NA MKEWE DKT SALLY WAMEUNGANA NA MSAFARA HUU KWA MARA NYINGINE? BILA SHAKA NI JAMBO LILILOPANGWA KWA MUDA!JEE UNA FIKRA YOYOTE KULIHUSU? TUANDAMANE NAO TUPATE KUSIKIA YATAKAYOJIRI..

**SCENE 2: COMMUNITY HALL**

**30.** ***SFX: A LOT OF BACKGROUND NOISE AND VOICES. THE HALL IS FULL OF PEOPLE, TAPPING OF HAND ON TABLE***

**31. CHIEF** Tunyamaze … sasa tunyamazeni sote…wageni wetu wamefika… ningependa kumkaribisha afisa mkuu wa huduma za afya ya Jamii, Edward Mwinga!

**32.** ***SFX: CLAPPING***

**33. EDDI** Ahsante sana bwana Chifu ..Ujumbe nilioandamana nao hivi leo, si wageni kwenu. Ni wenzetu katika jamii hii. Wengi wetu wanamfahamu Mama Sam ambaye hivi majuzi alifiliwa na binti yake baada ya kuugua ugonjwa wa kuhara.….

**34. CHIEF** **(interrupts)**Pole sana Edith…

**35. EDDI** Lakini kilichotuleta hapa, ni kwamba vifo vya aina hii vinaweza kuepukika.Ikiwa tutashirikiana kudumisha usafi wa mazingira yetu.

**36. CROWD:** **(overlapping)** Ni kweli ni kweli…Usafi ni sharti udumishwe.. na kisha sisi sote.…

**37. EDITH** **(whispering)** Maria.. Maria …Ni na wasi wasi… pengine halikuwa wazo zuri.

**38. MARIA** **(whispering)** Hautatatizika.. Ungependa kuona Mama mwengine akimpoteza mtoto wake?

**39. EDDI** Sasa nachukua nafasi hii kumkaribisha Edith azungumze machache …Mama Sam..!.

**40. SFX: CLAPPING**

**41. MARIA** **(firmly)** Nenda…. wanakusubiri…!

**42.** ***SFX CHAIR CREAKS.***

**43. EDITH** ***(clears throat)*** Mheshimiwa Chifu, nashukuru kwa kunipa muda huu.. nilimpoteza mototo wangu Fatu kwasababu ya ugonjwa wa kuhara.Tangu wakati huo, mimi na familia yangu pamoja na rafiki yangu Maria tumejifunza mengi kuhusu ugonjwa huu.Endapo tungekuwa tumeyafahamu mapema, labda Fatu angekuwa bado yu hai wakati huu.***(starts to fade out)*** Kwanza hatukufahamu kwamba tulipaswa kuzitupa mbali nepi chafu alizotumia mtoto na kisha kunawa mikono mara moja.Si makosa yetu kwani hata zamani hatukuwa tukifanya hivyo.

**44. NARRATOR** NA EDITH AKAENDELEA KUKISIMULIA KISA CHAKE:HATA HIVYO MANENO MATUPU HAYAWEZI KUUZUWIA UGONJWA WA KUHARA.NI VITENDO. FAMILIA HII NA RAFIKI ZAO WANATAKA JAMII NZIMA IJIFUNZE MBINU BORA ZA KUDUMISHA USAFI.HUU NDIO WAKATI WA KUCHUKUA HATUA.FURSA SASA NI YA DKT SALLY NA EDDI KUPANDA JUKWAANI.

**45. DR SALLY** Mabibi na mabwana ,na mheshimiwa Chifu,kama Daktari nina jambo moja tu la kuwaelezea.Vifo vingi vinaweza kuepukika.Kila mmoja wetu anaweza kuepuka maambukizi pamoja na kuvisambaza vijidudu na amiba vinavyosababisha ugonjwa huu wa kuhara.Hatua ya kwanza kabisa ni kumtibu kila mmoja ambaye ameambukizwa. Na hapo Bw Chifu tunahitaji mpango maalum.

**46. CHIEF** Mpango wa aina gani Dkt Sally?.

**47. DR SALLY** Mimi na mume wangu Eddi tumeandaa mkutano maalum ambapo watu wazima na watoto watapimwa kwa hiari ili kubaini iwapo wameambukizwa vijidudu vinavyosababisha ugonjwa huu.Baada ya hapo tutawatibu katika hospitali kuu ya umma

**48. SOUNDS:** ***CLAPPING***

**49. CHIEF** Ahsante sana..ahsante Dkt Sally. Naona Eddi amebahatika sana kumpata mke kama wewe!.!

**50. CHIEF:** Lakini mpango huo hauwezi kuutokomeza ugonjwa wa kuhara kijijini mwetu.. au sivyo?

**51. EDDI** Hapana, hautaweza kuumaliza. Na ndio sababu tanataka kuanzisha miradi ya kijamii.Kundi lililo katika hatari zaidi ya kuambukizwa ni watoto**.**Tunao vijana wawili hapa Sam na Chemu, ambao tayari wameanzisha miradi ya kuzuia ugonjwa huu shuleni mwao.

**52. MARIA** ***(interrupting soudly)*** Eddi,Kwani umenisahau. Mimi pia ningependa kushirikiana nao.

**53. CHIEF** ***(chuckling)*** Maria, Maria… Bado hujabadilika. Kila mara huachi vituko. Lakini nafurahi kwamba unatuunga mkono.!.

**54. MARIA** ***(with arrogance)*** Mimi pamoja na rafiki yangu hapa Edith tunapendekeza kuwa sisi kina mama wote katika kijiji hiki, tuwe tukikutana mara moja kwa mwezi, kupanga mikakati ya kudumisha usafi majumbani mwetu katika juhudi za kuzuia maambukizi.

**55 CROWD:** ***CLAPS***

**56 CHIEF** Vyema kabisa, Maria. Sasa mikutano hiyo ningependa kuona ikianza mara moja. Lakini sasa Eddi, hawa watoto jukumu lao ni gani.? Sam na Chemu watashirikishwa vipi?

57 **NARRATOR** NA KWELI JUKUMU LA WATOTO NI LIPI? WATOTO NDIO WALIO HATARINI KUAMBUKIZWA. WAKATI WANAPOKUA WADOGO WATOTO HUWA NA HAMU YA KUJIFUNZA MENGI NA MWISHOWE HUSHIKA KILA KILICHO KARIBU NAO. AGHALABU WANATIA VITU MDOMONI.WANAFUNZI NAO WANATANGAMANA SANA KILA WAKATI.KUTOKANA NA HILO UWEZEKANO WA KUVISAMBAZA VIDUDU NA VIMELEA VINAVYOSABABISHA KUHARA NI MKUBWA. MIRADI INAYOKUSUDIWA KUIEPUSHA HALI HII SHULENI NI MUHIMU SANA SHULENI. SAM NA CHEMU TAYARI WAMELITAMBUA HILO.KWA USHIRIKIANO NA JAMII, **CHIFU NA HATA FAMILIA ZAO , MIRADI HII INAWEZA KUANZA KUTEKELEZWA MARA MOJA.**

**SCENE 3: SAM/CHEMU SCHOOL. HEADMASTER'S OFFICE**

***58 SFX (IN THE BACKGROUND) SCHOOLCHILDREN PLAYGROUND NOISES***

**59 HEAD MASTER** Eddi na Dkt Sally, kama mwalimu mkuu wa shule hii, ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa kazi nzuri munayoifanya katika shule hii.

**60 EDDI** Ahsante kwa kutambua juhudi zetu Mwalimu mkuu. Lakini tunahitaji ushirikiano. Mke wangu hapa amejitolea kuiendeleza miradi hii ya kuangamiza ugonjwa wa kuhara..

**61 DR SALLY** Ni kweli lakini, pongezi za dhati zinapaswa kupewa watoto hawa wawili, Sam na Chemu. Lilikuwa wazo lao na hatimaye sote tumeshirikishwa!.

**62 HEADMASTER** Sam, Chemu, sisi tunajivunia sana ujasiri wenu. Mradi ule wa usimamizi bora wa misala umekuwa wa manufaa makubwa kwa kila mtu. Bila shaka nyinyi ni mfano mzuri wa kuigwa na wanafunzi wengine.

**63 SAM/CHEMU** Ahsante sana Mwalimu Mkuu**..**

**64 SAM** Na bado tuna mawazo mengine ya ubunifu mwalimu mkuu.

**65 HEADMASTER** Sam, Nakusikiliza.

**66 CHEMU** Tumetunga wimbo ambao tungependa kuwafunza wanafunzi wote hapa shuleni..

**67 HEADMASTER** Wimbo?

**68 SAM** Ndio kuhusu umuhimu wa kunawa mikono. Mimi na Chemu tutaanza ***Ku-Rap.***

**69 HEADMASTER** **Rap**?

**70 SAM/CHEMU**

*Wash your hands.*
*Only washed hands*
*should be used,*
*to eat.*
*Careless people,*
*Don't wash their hands*
*after visiting the toilet.*
*Keep healthy.*
*Wash your hands.*

**71 HEADMASTER** ***(Clapping)*** Kazi nzuri sana … nyinyi ni watoto werevu sana! Munaweza kuwafunza wenzenu wimbo huu hapo kesho wakati wa mkutano wa asubuhi.

**72 SAM** Na si hayo tu Mwalimu**.**

**73 HEADMASTER** Kuna wimbo mwengine?

**74 SAM** Hata si wimbo, bali ni mradi. Tunafikiria kuanzisha mradi ambapo kutumia nafasi yako, unaweza kuwaomba wanafunzi kukisimamia choo chochote kile katika jamii wanazoishi.

**75 HEADMASTER** Ndio …. Endelea nasikiliza!.

76 **EDDI** Mwalimu mkuu , hebu niwasaidie Sam na Chem.La msingi ni kwamba kwa vile wanafunzi hawa wamejifunza jinsi ya kusafisha vyoo hapa shuleni,tungependa wafanye hivyo pia nyumbani kwao.

**77 HEADMASTER** Wazo zuri sana. Ehhe endelea.

**78 SAM** Tungependa kuanzisha kundi.

79 **CHEMU** Na wanafunzii wote wahimizwe wajiunge na kundi hilo..

80 **HEADMASTER** Kundi lenyewe linaitwaje?

**81 CHEMU/SAM** Linaitwa *CTC.* The Clean Toilets Club.Kila mwanafunzi atachagua msala shuleni au kijijini mwake na kuhakikisha kuwa wote wanaoutumia wanakisafisha na kukiacha safi kila wakati. Mjomba Eddi atatusaidia.

**82 EDDI** Nitakuwa nikiandamana nao ili nipate kuzungumza na jamii na kuwapa maelezo. Sam na Chemu watahakikisha kuwa tuliyojifunza hapa yanatekelezwa.

**83 HEADMASTER** Vizuri, Vizuri…natamani wanafunzi wangu wote wangekuwa kama nyinyi Sam na Chemu**…(**PAUSE)… Nami pia nina wazo.

**84 EDDI** Wazo gani.

85 **HEADMASTER** Jee wewe Eddi na Dkt Sally munaweza kuandaa mijadala kuhusu suala hili la usafi angalau mara moja kwa mwezi? Yaani mchague maada muitakayo na sisi tutawaagiza wakusanyike wawasikilize.

86 **DR SALLY** Nadhani hilo pia ni wazo zuri..

87 **EDDI** Nadhani kazi yangu kama afisa wa huduma za afya ya jamii itakuwa imekamilika! Kwa kufanya hivyo mutakuwa munanirahisishia kazi hiyo!!

**BRIDGE MUSIC**

**OUTRO**

**88 NARRATOR** JAMII HII IMEPATA SI TUU NGUVU MPYA YA NJIA BORA ZA KUDUMISHA USAFI BALI PIA MAISHA BILA HATARI YA KUAMBUKIZWA UGONJWA WA KUHARA.NAO SAM NA CHEMU WAMEKUWA MABALOZI WA AFYA BORA KATIKA JAMII.

NA WEWE JEE? NINI UNACHOWEZA KUKIFANYA KATIKA JUHUDI ZA KUSAIDIA KUPAMBANA NA JANGA HILI? LABDA UNAWEZA KUWASAMBAZIA MARAFIKI UJUMBE ULIOJIFUNZA KATIKA VIPINDI HIVI VYOTE KUMI VYA NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO ULIVYOVISIKILIZA.TUJITAHIDI KUDUMISHA USAFI NA KUZIIMARISHA AFYA ZETU KWANI KWA KUFANYA HIVYO TUTAKUWA TUNALISAIDIA BARA LA AFRIKA KUPUNGUZA IDADI YA VIFO AMBAVYO VINAWEZA KUEPUKIKA.

NA HAPO NDIPO TUNAPOFIKA MWISHO WA MFULULIZO HUU WA VIPINDI VYA NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO KUHUSU USAFI NA KINGA DHIDI YA UGONJWA WA KUHARA.MAKALA HAYA YAMEANDIKWA NA NJOKI MUHOHO.UKIPENDA KUSIKILIZA TENA VIPINDI VYA NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO TAZAMA MTANDAO WETU WA WWW.DW-WORLD.DE/LBE. UNAWEZA PIA KUTUMA MAONI YAKO KUHUSU YOTE ULIYOJIFUNZA. HADI WAKATI MWENGINE KWAHERI KWA SASA.